Serikali yaombwa kuingilia kati bei ya nyama

Na Steven Augustino,Tunduru

■■SERIKAli imeombwa kuingilia kati na kuhakikisha bei ya kitoweo cha nyama ya ng'ombe kinapungua bei ili na kuwafanya wananchi kupata unafuu hasa kipindi cha Sikukuu ambacho uhita wake huwa ni mkubwa.

Kilio hicho kimetolewa na baadhi ya wananchi wa Mji wa Tunduru Mkoani Ruvuma walipokuwa wakizungumza na Majira juzi kuhusiana na bei kubwa ya nyama inayouzwa na wafanyabiashara wa mji huo.

Walisema katika kipindi kirefu wafanyabiashara hao wanaomiliki maduka ya kuuzia nyama ya ng'ombe wamekuwa wakiwauzia kwa bei ya sh 8,000 kwa kilo moja ikiwa ni tofauti na maeneo jirani ikiwemo makao makuu ya mkoa ambako huuzwa kati ya shilingi 6,000 na 5,000 kwa kilo moja.

Mwajuma Hamisi na Japhet Mnyagala walisema kuwa awali bei hiyo ilionekana ni ya kawada lakini hata baada ya miundombinu ya barabara kufunguka bado bei hiyo kubwa inaendelea.

"Wakati barabara ikiwa ya vumbi tulioina hali hiyo kuwa ni ya kawaida, lakini hivi sasa barabara ya lami imeshajengwa na kuwapunguzia usumbufu lakini bei haipungui," alisisitiza Mnyagala na kuongeza kuwa hali hiyo inawafanya wananchi kushindwa kumudu gharama hiyo na kutoweza kula nyama.

Wakizungumzia hali hiyo baadhi ya wafanya biashara wa maduka ya nyama ya ng'ombe mjini hapa, Salama Anosisye na Caesar Luambano Nyamka walisema kuwa hali hiyo inasababishwa serikali kuwazuwia kuingiza ng'ombe wa kuchinja kutoka nje ya wilaya hiyo.

Walisema kutokana na wafanyabishara hao kuongezeka huku wakiwa wanashindana kutoka Wilaya za Masasi, Nanyumbu, Nachingwea na Newale wanaouzwa katika mnada mmoja uliopo katika Kata ya Muhuwesi Wilayani Tunduru ambapo bei ya ng'ombe hununuliwa kwa bei kubwa ambayo huwafanya washindwe kuuza chini ya bei ya sh. 8,000.

Walisema Wilaya ya Tunduru inao wafugaji wachache ambao wamesambaa katika maeneo ya Tarafa za Matemanga, Lukumbule, Nalasi, Namasakata lakini wamekuwa wakishindwa kupeleka mifugo yao katika mnada mmoja ambao upo tarafa ya Nakapanya.

Walisema kikwazo kingine ni pamoja na kuwepo kwa zuwio hilo pia wafanyabiashara hao kuzuiliwa kununua ng'ombe nje ya eneo la mnada hali hiyo pia imekuwa ikiwapa mazingira magumu ya utekelezaji wa majukumu hayo ya kuwa hudumia wananchi kupata kitoweo chenye unafuu wa bei.

Mkuu wa Wilaya ya Tunduru Mkoani Ruvuma, Julius Mtatiro amekiri kuwepo kwa changamoto hiyo na kwamba tayari ameanza kuifanyia kazi kwa kuwaita wafanyabiashara hao na kuzungumza nao kwa lengo la kutafuta suluhu ya kudumu.

UZA, NUNUA KITU CHENYE THAMANI KUBWA KWA KUTANGAZA NASI KWA SIMU: 0754 852 730

VIWANJA
Vinauzwa vipo maeneo ya Tabata, Mbagala, Temeke, Msasani, Salasala, Kisemvule, Mabwepande na maeneo mengine.
Simu: 0683246695

NYUMBA
Inauzwa iko Tabata Bima st.Mary ina vyumba 3 kimoja master, nyuma kuna mabanda 2 ina hati miliki bei yake milioni 90 pia viwanja vinauzwa viko Goba ukubwa mita 50x22 na kingine 30x25 bei milioni 30.
Simu: 0715027571

ENEO
Linauzwa liko Kinzudi kwa
Simu: 0715027571

NYUMBA
Inauzwa iko Kinzudi Goba ina vyumba 3 kimoja master, sitting dinning, jiko, stoo uwanja wake mita 30x30 maji na umeme yapo bei milioni 60 na mazumgumzo yapo.
Simu: 0715027571

SHAMBA
Linauzwa lipo Tabata Bima bei ni milioni 60 pia shamba linauzwa Vikindu, bei ni milioni 55 na Kisemvule. **Simu:** 0683246695.

MGAHAWA
Unakodishwa upo Kariakoo kodi milioni 1.2 na upose hemu nzuri sana panafaa kwa biashara.

KIWANJA
Kinauzwa kipo Tabata bei ni nafuu sana na maelewano yapo.
Simu: 0745 744820

SHAMBA
Hekari tatu na nusu linauzwa lipo Mwanambaya-Mizugu Wilaya ya Mkuranga. Bei ni milioni 25.Maelewano yapo
Simu: 0715 919551.

NYUMBA
Inapangishwa ipo Kijitonyama i vyumba 3, masta, sitting, dining fensi bei ni maelewano.
Simu: 0742 360099

PLOT KUBWA
Inauzwa ipo Kitunda relini nyu

Scanned by CamScanner

Wafugaji wakaidi kuosha mifugo kukiona

Na Jumbe Ismailly, DODOMA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imeziagiza kamati za majosho kutunga sheria ndogo zitakazosimamia na kuwadhibiti wafugaji wanaokwepa kupeleka mifugo yao kuogesha kwa lengo la kukabiliana na magonjwa yatokanayo na kupe.

Agizo hilo limetolewa na Kaimu Ofisa Mfawidhi kituo cha uchunguzi wa magonjwa ya mifugo Kanda ya Kati, Dk. Samuel Mngumi, wakati wa uzinduzzi wa awamu ya pili ya kampeni za uogeshaji mifugo Kanda ya Kati uliofanyika katika Kijiji cha Mkoyo, Kata ya Hombolo, mkoani Dodoma.

Alisisitiza kwamba kamati za majosho ndiyo moyo wa majosho na shughuli nzima za uogeshaji, hivyo waweke sheria ndogo za kuwajibishana ili utaratibu wa kuogesha uwe endelevu. Dk. Mngumi alisema kwamba anaamini kuwa kila halmashauri imetunga sheria zake ndogo kwa baadhi ya wafugaji wachache wanaokaidi kupeleka mifugo yao kwenda kuogesha wanavyoshughulikiwa ili wasiwakatishe tamaa wafugaji wengine wenye moyo wa kupambana na magonjwa yanayotokana na kupe.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, kuna sheria nyingi zinazoongoza udhibiti wa magonjwa ya mifugo kwa sababu magonjwa yanasababishwa na virusi vingi na kutoa mfano wa sheria ya magonjwa ya wanyama ya mwaka 2003 inayoeleza kwamba ni lazima watu washiriki katika kudhibiti magonjwa.

Alieleza kuwa baada ya serikali kuona kwamba upo uwezekano kwa baadhi ya wafugaji kuwa wazito kutekeleza agizo hilo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipo katika hatua za mwisho za kutoa kanuni za udhibiti wa magonjwa ya mifugo kwenye baadhi ya maeneo.

"Kwa mfano kuna kanuni ya kuogesha itatoka, na itazungumzia habari za kuogesha tu, kwamba mtu asipoogesha kuna mambo gani yatafanywa, mtu afanyweje na kadhalika, lakini kuna kanuni nyingi kulingana na juhudi za kudhibiti magonjwa," alibainisha.

Naye daktari wa mifugo wa Jiji la Dodoma, Innocent Peter, alisema kwamba tangu kampeni ya uogeshaji zilipoanza zimepunguza matukio ya magonjwa yanayotokana na kupe kulinganisha na kabla ya kampeni hiyo kuanza.

Alisema hivi sasa matukio ya magonjwa yatokanayo na kupe kwa ng'ombe na mbuzi yamepungua kutoka 30 kwa mwezi yaliyokuwapo kabla ya kampeni hadi matukio kati ya matano hadi 10 kwa mwezi kwa maeneo ya vijijini wakati kwa wafugaji wa maeneo ya mjini simu walizokuwa wakipigiwa na wafugaji wao zimepungua.

Mmoja wa wafugaji waliohudhuria uzinduzi wa kampeni hiyo Yoro Losiwa, alisema kwamba kampeni hiyo ni nzuri kwani inalenga kupunguza na kama siyo kutokomeza kabisa magonjwa yatokanayo na kupe.

Mwenyekiti wa serikali ya Mtaa wa Mkoyo, Benjamini Lebolo, alishukuru serikali kwa kuliona suala la majosho ambalo linalolenga kupunguza na kama siyo kumaliza kabisa vifo vya mifugo.

Scanned by CamScanner

KAMPENI>> Magonjwa ya kupe yamepungua kutoka 30 hadi matano

Wafugaji wanaokwepa kuogesha mifugo yao kwenye majosho kuchukuliwa hatua

NA JUMBE ISMAILLY, Dodoma

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imeziagiza kamati za majosho kutunga sheria ndogo zitakazosimamia na kuwadhibiti wafugaji wanaokwepa kupeleka mifugo yao kuogesha kwa lengo la kukabiliana na magonjwa yatokanayo na kupe.

Agizo hilo lilitolewa na Kaimu Ofisa Mfawidhi Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo, Kanda ya Kati, Dk. Samwel Mngumi, wakati wa uzinduzi wa awamu ya pili ya kampeni za uogeshaji mifugo Kanda ya Kati, uliofanyika katika Kijiji cha Mkoyo, Kata ya Hombolo, mkoani Dodoma.

Dk. Mngumi alisema kamati za majosho ndiyo moyo wa majosho na shughuli nzima za uogeshaji, hivyo waweke sheria ndogo za kuwajibishana ili zoezi la kuogesha liwe endelevu.

Akifafanua, alisema kila halmashauri imetunga sheria zake ndogo kwa baadhi ya wafugaji wachache wanaokaidi kupeleka mifugo yao kwenda kuogesha.

Dk. Mngumi alisema hatua zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya watu hao ili wasiweze kuwakatisha tamaa wafugaji wengine wenye moyo wa kupambana na magonjwa yanayotokana na kupe.

Kwa mujibu wa daktari huyo wa mifugo, kuna sheria nyingi zinazoongoza udhibiti wa magonjwa ya mifugo, kwa sababu yanasababishwa na vitu vingi.

Alitoa mfano wa Sheria ya Magonjwa ya Wanyama mwaka 2003, inayoeleza kwamba ni lazima watu washiriki katika kudhibiti magonjwa kwa ujumla.

"Kuna sheria yetu ya magonjwa ya mifugo ya mwaka 2003. Sheria ya Wanyama ya mwaka 2003, inaeleza kabisa kwamba, lazima watu washiriki katika kudhibiti magonjwa, lakini kuna kanuni zake pia za mwaka 2007," alisisitiza.

Dk. Mngumi aliweka bayana kuwa, baada ya serikali kuona upo uwezekano kwa baadhi ya wafugaji kuwa wazito kutekeleza agizo hilo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipo katika hatua za mwisho za kutoa kanuni za udhibiti wa magonjwa ya mifugo kwenye baadhi ya maeneo.

Daktari wa Mifugo wa Jiji la Dodoma, Innocent Peter, licha ya kuishukuru serikali kwa kuona umuhimu wa kufufua huduma za majosho, alisema tangu kampeni hizo za uogeshaji zilipoanza, zimepunguza matukio ya magonjwa yanayotokana na kupe.

Alisema kuwa hivi sasa matukio ya magonjwa yatokanayo na kupe kwa ng'ombe na mbuzi, yamepungua kutoka 30, kwa mwezi, yaliyokuwepo kabla ya kampeni hadi kufikia matukio kati ya 5 hadi 10, kwa mwezi, kwa maeneo ya vijijini, wakati kwa wafugaji wa maeneo ya mjini simu walizokua wakipigiwa na wafugaji hao zimepungua.

"Kama daktari wao wa mifugo, nawataka wafugaji waendelee kuleta mifugo yao zaidi na kuwahamasisha wale ambao hawaleti mifugo yao kuogesha. Nafahamu kwenye kijiji wanafahamiana kwani kama mfugaji haleti kuogesha, atakuwa chanzo cha kusambaza kupe kwa wafugaji ambao wanaleta mifugo," alibainisha daktari huyo.

Kwa upande wao, baadhi ya wafugaji waliohudhuria uzinduzi wa kampeni hiyo ya uogeshaji awamu ya pili, akiwemo Yoro Losiwa, aliweka bayana kwamba kampeni hiyo ni nzuri kwani inalenga kupunguza kama sio kutokomeza kabisa magonjwa yatokanayo na kupe.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mkoyo, Benjamini Lebolo, alitumia fursa hiyo kuipongeza serkali na waziri mwenye dhamana ya mifugo na uvuvi, kwa kuliona suala la majosho linalolenga kupunguza kama sio kumaliza kabisa vifo vya mifugo.

Scanned by CamScanner